## HALMASHAURI YA WILAYA YA MULEBA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA WATALAAMU (CMT) KILICHOFANYIKA TAREHE 13/01/2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA.**

**A. Mahudhurio ya Wajumbe**

| NA | JINA KAMILI | CHEO /WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Shaban F. Manyama | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Essery F. Pima | Katibu |
| 3 | Ndg. Emmanuel Masha | Mjumbe |
| 4. | Ndg. Alistides Kyobya | Mjumbe |
| 5. | Dr. Abdillian Fransis | Mjumbe |
| 6. | Ndg. Keneth A. Mariro | Mjumbe |
| 7. | Ndg.Robert Josephat | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Henrrietha William | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Zephania Chacha | Mjumbe |
| 10. | Ndg. Lucy A. Binamungu | Mjumbe |
| 11. | Ndg. Evart Kagaruki | Mjumbe |
| 12. | Ndg. William Ferdinand | Mjumbe |
| 13. | Ndg. Charles L. Ntaki | Mjumbe |
| 14. | CPA. Revocatus Manyerere | Mjumbe |
| 15. | Ndg. Jared Muhile | Mjumbe |
| 16. | Ndg. Johaiveni Kyaruzi | Mjumbe |
| 17. | Ndg. Veronika Kanifes | Mjumbe |
| 18. | Ndg. Leonard N. Ndyakowa | Mjumbe |
| 19. | Ndg. Kagoroba Damas | Mjumbe |
| 20. | Ndg. Amini Kijwile | Mjumbe |
| 21. | Ndg. Avith C. Mushobozi | Mjumbe |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| . | Ndg. Amad A. Khalfan | Mjumbe |
| . | Ndg. Michael Mbembela | Mjumbe |
| . | Ndg. Nestory Mkama | Mjumbe |
| | Ndg. Jonas Rutaraka | Mjumbe |
| | Ndg. Elly Muga | Mjumbe |

**B. SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| | Ndg. Aziza Rashidy | Katibu wa Kamati |

**C. AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAMU (CMT) KILICHOFANYIKA TAREHE 13/01/2022**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUTHIBITISHA AGENDA
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 10/12/2021
4. YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 10/12/2021
5. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI YA WILAYA KUISHIA MWEZI DISEMBA, 2021
6. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA -DISEMBA, 2021/2022
7. TAARIFA ZA IDARA
   i. Idara ya Utawala na Utumishi
   ii. Idara ya Elimu Msingi
   iii. Idara ya Elimu Sekondari
   iv. Idara ya ya Afya
   v. Idara ya Ardhi na Maliasili
   vi. Idara ya Kilimo, Uwagiliaji na Ushirika
   vii. Idara ya Mifugo na Uvuvi
   viii. Idara ya Maendeleo ya Jamii
   ix. Idara ya ujenzi
   x. Mamlaka ya Mji Mdogo Muleba
   xi. Taarifa za Utekelezaji wa shughuli za Uthibiti Ubora wa Shule katika kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022
   xii. Kitengo cha sheria
   xiii. Kitengo cha manunuzi
   xiv. Kitengo cha usafirishaji
   xv. Kitengo cha TEHAMA
   Kitengo cha Biashara
   xvi. MLUWASA
   xvii. Idara ya Mipango

Wajumbe waliagiza kuwa Mweka Hazina na Mwanasheria kuhakikisha "Control number" inatolewa na kupewa HTT ili waweze kulipa deni lao.

Mwenyekiti alisisitiza kutumika kwa fedha za bakaa ili zlishe kulingana na bajeti ilivyopangwa.

Wajumbe walishauri kuhusu vyanzo vyote vya mapato vilivyokusanya chini ya asilimia vifuatiliwe ikiwemo na meza sokoni.

Wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021/2022.

**MUHT. NA. 72/2021/2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA ROBO YA PILI OKTOBA - DISEMBA, 2021/2022**

Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliwasilishwa na Kaimu Afisa Mipango ikionesha shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021/2022 kwamba:-

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri iliidhinishiwa jumla ya Tshs. 21,582,051,909.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Tshs. 2,568,377,043.00 ni mchango wa Halmashauri kutokana na mapato ya ndani na Tshs. 19,013,674,866.00 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu.

**MAPOKEZI NA MATUMIZI YA FEDHA**

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2021, jumla ya Tshs. 868,810,273.82 sawa na asilimia 27.19 zilipokelewa. Kati ya hizo, Tshs. 5,103,424,872.17 sawa na asilimia 26.84 ni kutoka Serikali Kuu na Tshs. 765,385,401.65 sawa na asilimia 29.80 ni mchango wa Halmashauri ya Wilaya. Aidha, Halmashauri ilitumia jumla ya Tshs. 3,964,897,638.55 na kubakia na Tshs. 1,903,912,635.27.

**FEDHA ZILIZOVUKA MWAKA (BAKAA 2020/2021)**

Katika kipindi hiki, Halmashauri ilikuwa na salio la Tsh. 159,610,637.00 zikiwa ni fedha za miradi iliyovuka mwaka 2020/2021. Hadi kufikia 31 Disemba, 2021 Halmashauri ilitumia jumla ya Tshs. 127,716,797.4 na kubakia na Tshs. 31,893,838.60.

**MAPOKEZI NJE YA BAJETI**

Hadi kufikia 31 Disemba, 2021, Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. 5,961,600,840.00 nje ya bajeti na kuzigawa kwa walengwa kama ifuatvyo;- TASAF kiasi cha Tshs. 100,290,000.00, Grobal Fund UKIMWI kiasi cha Tshs. 4,796,093.00, Afya kaisi cha Tshs. 250, 000,000.00, idara ya Elimu Sekondari kiasi cha Tshs. 100,000,000.00, idara ya Elimu Msingi kiasi cha Tshs. 100,000,000.00, ujenzi wa madarasa 208 shule za Sekondari (UVICO-19) kiasi cha Tshs. 4,160,000,000.00, ujenzi wa shule shikizi 26 za msingi (COVID -19) kiasi cha Tshs. 520,000,000.00, ujenzi wa bweni shule ya msingi Kagondo kiasi cha Tshs. 80,000,000.00, uboreshaji kituo cha Afya Kamachumu 250,000,000.00,



CamScanner

Idara ya Elimu Msingi inaundwa na vitengo vya Taaluma, Vifaa na Takwimu, Elimu ya Watu Wazima, Elimu Maalum pamoja na Utamaduni na michezo. Kwa sasa idara hii ina jumla ya shule za msingi 245 (230 za Serikali na shule 15 za binafsi) zikiwa na jumla ya wanafunzi 175,032 [Wavulana 87,224 na Wasichana 87,808] kuanzia elimu ya awali hadi darasa la saba. Shule za msingi za Serikali zina wanafunzi wapatao 171,994 [wavulana 85,641 wasichana 86,353] sawa na mahitaji ya walimu 4,148 wakati waliopo ni 2,268 na upungufu ni walimu 1,880. Kwa upande wa shule zisizo za Serikali wapo wanafunzi wapatao 3,038 [wavulana 1,583 wasichana 1,455] na kufanya mahitaji ya walimu kuwa 76 wakati waliopo ni walimu 82 hivyo hakuna upungufu katika shule za binafsi.

Utengenezaji wa madawati 500 ambayo yalitengenezwa kupitia mapato ya ndani yenye thamani ya milioni thelathini (30,000,000/=) katika kituo cha shule ya msingi Ngenge. Madawati haya yatagawiwa kwenye shule zenye upungufu mkubwa wa madawati.

Bati 2319 zimenunuliwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa na nyumba ya mwalimu katika shule ya msingi Msalala. Bati hizo zina thamani ya Tshs. 70,777,503.00 (ununuzi Tshs. 66,672,873 na usafirishaji Tshs. 4,104,630).

Mapokezi ya vyeti vya wahitimu darasa la saba, vyeti 58,779 viliandaliwa kwa wahitimu wa darasa la saba kuanzia mwaka 2008 hadi 2016 na vinaendelea kusainiwa.

Usajili wa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza kwa mwaka 2022, maoteo ya wanafunzi wa elimu ya awali yalikuwa 19,634 (wavulana 9,834 na wasichana 9,800). Hadi sasa wamesajiliwa wanafunzi 13,010 (wavulana 6,206 na wasichana 6,804) sawa na 68%. Kwa darasa la kwanza maoteo yalikuwa jumla 17,274 (wavulana 8,592 wasichana 8,682). Wanafunzi 11,704 wamesajiliwa (wavulana 5602 wasichana 6102) sawa na 68%.

Kupokea fedha kiasi cha Tshs. 445,807,303.89 kwa ajili ya shughuli mbalimbali kwa shule 227. Kiasi cha Tshs. 136,200,000 kilipokelewa kwa ajili ya posho ya Walimu Wakuu 227, kiasi cha Tshs 31,500,000/= kilipokelewa kwa ajili ya Maafisa Elimu Kata 42, kiasi cha Tshs 49,407,463.56 kilipokelewa kwa ajili ya shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum na kiasi cha Tshs. 228,699,840.3 kilipokelewa kwa ajili ruzuku ya uendeshaji wa shule (Capitation).

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya Elimu Msingi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021/2022.

## III. IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Taarifa ya idara ya Elimu Sekondari iliwasilishwa na Afisa Elimu Sekondari ikionesha shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Disemba, 2021 kama ifuatavyo;-

Halmashauri ya wilaya ya Muleba ina jumla ya shule za sekondari 55, ikiwa shule 40 ni za Serikali na shule 15 ni za binafsi zenye jumla ya wanafunzi 33,865 ambapo wavulana ni 16,069 na wasichana 17,796. Idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ni 29,821 ambapo wavulana ni 14,073 na wasichana ni 15,748. Shule za binafsi zina jumla ya wanafunzi 4,044 ambapo wavulana ni 1,996 na wasichana ni 2,048. Walimu waliopo n 699 ambapo walimu wa kike ni 176 na wa kiume ni 523.

Shughuli zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na uratibu wa ufanyikaji wa mtihani wa upimaji Kitaifa kidato cha pili na mtihani wa kuhitimu elimu ya kidato cha nne mwaka 2021. Mtihani wa kidato cha pili ulianza tarehe 01.11.2021 na kukamilika tarehe 11.11.2021. Katika Wilaya ya Muleba jumla ya shule 54 zilifanya mtihani huo ikiwa shule za Serikali 39 na shule za binafsi 15. Mtihani wa kidato cha nne ulianza tarehe 11.01.2021 na kukamilika tarehe 02.12.2021. katika wilaya yetu ya Muleba shule zilizoshiriki mtihani huo ni shule 53 ikiwa shule 39 ni za Serikali na shule 15 ni za binafsi.

Usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa fedha za UVIKO-19 ambapo Serikali ilituma Tsh.4,160,000,000.00. Fedha hizo ziliingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule za sekondari tarehe 21.10.2021.Ujenzi wa vyumba 208 vya madarasa katika shule za sekondari umekamilika.

Usimamizi na ufuatiliaji wa ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwa fedha za tozo ya miamala ya simu ambapo Serikali ilileta Tshs.100,000,000.00. Fedha hizo zilikuja kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 8 vya madarasa katika shule za sekondari 8 ambapo ujenzi umekamilika.

Usimamizi na ufuatiliaji wa ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwa fedha za Serikali Kuu ambapo Serikali ilileta kiasi cha Tshs.225,000,000.00. Fedha hizo zilikuja kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 18 vya madarasa katika shule za sekondari 16 ambapo ujenzi umekamilika.

kuratibu ujenzi wa shule tatu za sekondari za Mafumbo, Mushabago na Karambi kwa fedha za SEQUIP ambapo Serikali ilituma Tsh.1,410,000,000.00. Fedha hizo zimetumwa kwenye akaunti ya shule Nyakatanga Tsh. 470,000,000.00, Ikondo Tshs. 470,000,000.00 na Kagoma Tshs. 470,000,000.00.

Baada ya taarifa kuwasilishwa, mjumbe alihoji mikakati ya kuongeza walimu baada ya kuongeza shule mpya na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa ilishaandikwa barua kwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI ili waweze kutupatia walimu.

Wajumbe walishauri idara ya sekondari ihakikishe inaweka mikakati ya kuongeza samani.

Kwa pamoja wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya idara ya Elimu Sekondari kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021/2022.

## IV. IDARA YA AFYA

Taarifa ya idara ya Afya iliwasilishwa na Kaimu Mganga Mkuu ikionesha shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021 kama ifuatavyo;-

Wilaya ina jumla ya vituo vya huduma 47 ambapo vituo vya Serikali ni 32 kati ya vituo hivyo kuna hospitali 3 ambapo hospitali moja ni hospitali teule ya Wilaya (Rubya DDH). Kuna vituo vya afya 7 na zahanati 37.

Sekta ya baba, mama na mtoto ilifanya shughuli za kutoa huduma za mkoba, huduma za uzazi na mtoto, huduma za uzazi wa mpango na huduma za kujifungua. Kutoa elimu ya afya na kufanya upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi kwa jumla ya wanawake 15,055.



CamScanner

Kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kagondo. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 40,000,000/= toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19, kusimamia ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika shule ya sekondari Kamachumu. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 80,000,000/= toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19, kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya sekondari Mayondwe. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 40,000,000/= toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika shule ya sekondari Ngenge. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 80,000,000/= toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa katika shule ya sekondari Nyailigamba. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 100,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19 zimetumika.

Kusimamia ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa katika shule ya sekondari Nyakatanga. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 100,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19, kusimamia ujenzi wa vyumba saba vya madarasa katika shule ya sekondari Ruhanga. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 140,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika shule ya sekondari Rutabo. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 80,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba saba vya madarasa katika Shule mpya tarajiwa ya Sekondari katika kata Kagoma. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs 140,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19, kusimamia ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Ikuza. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 60,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19, kusimamia ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Mazinga. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 60,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19 zimetumika.

Kusimamia ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Kishanda. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 100,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba saba vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Kyebitembe. Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji. Fedha Tshs. 140,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Izigo. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 100,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba sita vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Ibuga. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 120,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba sita vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Kasharunga. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 120,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19 zimetumika.

Kusimamia ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Kimwani. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 100,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba sita vya madarasa katika shule mpya tarajiwa ya sekondari katika Kata Ngenge. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 120,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa bweni moja la wanafunzi shule ya msingi Kagondo. Ujenzi upo katika hatua ya umaliziaji. Fedha Tshs. 80,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya msingi shikizi Kisha. Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji.



CamScanner

Fedha Tshs 40,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya msingi shikizi Mashasha. Ujenzi upo hatua ya ukamilishaji. Fedha Tshs 40,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa shule ya msingi shikizi Daraja nane. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 80,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19 zimetumika.

Kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya msingi shikizi Kasenyi. Ujenzi umekamilika. Fedha Tshs. 40,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa vyumba saba vya madarasa shule ya msingi shikizi Maigabiri. Ujenzi upo katika hatua ya umaliziaji. Fedha Tshs. 140,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kuandaa michoro na BOQ kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura (EMD) na nyumba ya watumishi (3 in 1). Ujenzi upo katika hatua ya manunuzi. Fedha Tshs. 390,000,000.00 toka Shirika la IMF fedha za UVIKO-19,kusimamia ujenzi wa majengo ya maabara, jengo la upasuaji, jengo la mama na mtoto na jengo la kuhifadhia maiti katika kituo cha Afya Nshamba. Ujenzi upo hatua ya kupaua. Fedha Tshs. 400,000,000.00 toka fedha za tozo za miamala ya simu,kusimamia ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo cha Afya Izigo. Ujenzi upo hatua ya lenta. Fedha Tshs. 100,000,000.00 toka fedha za tozo za miamala ya simu.

Kuandaa michoro na BOQ kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule mpya tarajiwa tatu za sekondari za Kata chini ya mpango wa SEQUIP. Nyaraka hizo zimewasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa ajili ya hatua zaidi. Kutoa vibali vya ujenzi wa majengo. Vibali 14 vilitolewa.

Wajumbe waliipokea na kuipitisha taarifa ya idara ya Ujenzi kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021/2022.

## X. MAMLAKA YA MJI MDOGO

Taarifa ya Mamlaka ya Mji Mdogo iliwasilishwa na Kaimu Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo ikionesha shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2021/2022 kama ifuatavyo;-

Uendeshaji wa vikao vya kisheria, ukusanyaji wa mapato toka katika vyanzo vya ndani vya Mji Mdogo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ufuatiliaji wa usafi wa mazingira.

Ukusanyaji wa mapato toka vyanzo vya ndani vya Mamlaka ya Mji Mdogo, Mamlaka ya Mji Mdogo kwa mwaka 20212022 ilikisia kukusanya kiasi cha Tshs. 374,179,000.00 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2021, Mamlaka ya Mji Mdogo ilikusanya kiasi cha Tshs. 94,624,180.00 sawa na asilimia 25 ya lengo la mwaka. Kuanzia Julai 2021 hadi Disemba 2021, Mamlaka ya Mji Mdogo ilikusanya Tshs. 182, 328,931.00 sawa na asilimia 49 ya lengo la mwaka.

Kwa mwaka 2021/2022 Mamlaka ya Mji Mdogo ilikisia kutumia kiasi cha Tshs. 40,670,000.00. Kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2021, Mamlaka ya Mji Mdogo ilitumia Tshs. 3,900,000.00 sawa na asilimia 10. Kuanzia Julai 2021 hadi Disemba 2021, Mamlaka ya Mji Mdogo ilitumia kiasi cha Tshs. 10, 170,461.00 sawa na asilimia 28 ya lengo la mwaka.



CamScanner

**MUHT.NA.84/2021/2022 KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano. Kisha alifunga kikao mnamo saa 4:35 usiku.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA**

| | |
|---|---|
| **JINA.** Amani A Uhalfan | **JINA.** Essery F. Pima |
| **SAINI.** ……………………… | **SAINI.** ……………………… |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE:** 14/02/2022



CamScanner